



# Tom muuza ndizi

- ✍ Humphreys Odunga
- 👤 Zablon Alex Nguku
- 💬 Matteo E. Mwita
- 🗣 Kiswahili
- 📊 Level 2



Tom anabeba tenga la ndizi zilizoiva.



Tom anaenda sokoni kuuza ndizi.



Sokoni watu wananunua matunda.



Lakini hakuna anayenunua ndizi za Tom. Wanapenda kununua matunda kutoka kwa akina mama.



“Kwenye jamii yetu, ni wanawake pekee ndio wanaouza matunda,” watu wanasema. “Ni mwanamume wa aina gani huyu?” watu wanahoji.



Lakini Tom hakati tamaa. Anaita,  
“Nunua ndizi zangu! Nunueni ndizi  
zangu tamu zilizoiva!”



Mwanamke mmoja anachukua kichana cha ndizi kutoka kwenye tenga. Anaziangalia ndizi kwa umakini.



Mwanamke ananunua ndizi.



Watu wengine wanakuja kwenye kichanja. Wananunua ndizi za Tom na kuzila.



Mara, tenga linakuwa tupu. Tom  
anahesabu pesa alizopata.



Tom ananunua sabuni, sukari, na mkate. Anaweka vitu kwenye tenga lake.



Tom anajitwisha tenga kichwani na kwenda nyumbani.



# Storybooks Canada

[storybookscanada.ca](http://storybookscanada.ca)

## Tom muuza ndizi

Written by: Humphreys Odunga

Illustrated by: Zablon Alex Nguku

Translated by: Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook ([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) and is brought to you by [Storybooks Canada](http://Storybooks Canada) in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons  
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).